



Ili kuhamisha serikali katika hatua inayofuata ya [Mpango wa Kuanza Salama wa MI](#), Gavana Whitmer alisaini [Agizo Kuu la Utendaji 2020-110](#) mnamo Juni 1, 2020. Kwa jumla, agizo hili haliitaji tena Wakazi wa Michigan kubaki nyumbani, inaruhusu wauzaji kufungua Juni 4 na mikahawa kufunguliwa tena mnamo Juni 8, zote mbili chini ya mipaka ya uwezo. Kulingana na Gavana Whitmer, “Takwimu zimeonyesha kuwa tuko tayari kwa uangalifu kuhamisha jimbo letu kwenye hatua inayofuata ya [Mpango wa Kuanza Salama wa MI](#) [MI Safe Start Plan](#), lakini tunawajibika kwa mashujaa wetu wa mstari wa mbele kupata haki hii.” Isipokuwa itakapothibitishwa vingine, agizo linafaa kutekelezwa kwa mara moja.

MUHTASARI WA AGIZO LA UTENDAJI

- Sharti ya kukaa nyumbani isipokuwa kwa mahitaji ya kazi muhimu au kwa madhumuni mengine yanayoruhusiwa hayatumiki tena.
- Lazima uendelee kuvaa vifuniko vya uso (ikiwa na uwezo wa kimatibabu) unapokuwa katika nafasi zilizowekwa kwenye umma na unapaswa kuendelea kuchukua tahadhari zote nzuri za kujikinga ikiwa ni pamoja na kutunza nafasi ya miguu 6 kutoka kwa watu wengine.
- Kazi yoyote ambayo inaweza kufanywa kwa mbali (bila mfanyakazi kutoka nyumbani) lazima iendelee kufanywa kwa mbali.
- Biashara yoyote ambayo inahitaji wafanyakazi wake kuondoka nyumbani kwa kazi iko chini ya sharia ya usalama ya kazini katika [EO 2020-97](#) au amri yoyote ambayo itakayofuata.
- Duka za rejareja zinaweza kuanza na shughuli za kawaida mnamo Juni 4, 2020 kulingana na kanuni za mitaa na vizuizi vya uwezo na kiwango cha mahali pa kazi kinacoelezewa katika [EO 2020-97](#) au amri yoyote inayoweza kufuata.
- Mikahawa, mahakama ya vyakula, nyumba za kahawa, baa, na vilabu vya pombe zinaweza kufunguliwa tena kuanzia Juni 8 kwa makao katika nafasi ya ndani na nje kulingana na vikwazo vya viwango vya mahali pa kazi vinavyoelezewa katika [EO 2020-97](#) au amri yoyote ambayo itakayofuata.
- Mabwawa ya kuogelea (chini ya kiwango cha uwezo wa 50%) na kambi za mchana za watoto zinaweza kufunguliwa tena mnamo Juni 8
- Viwanja vya nje na vifaa vya starehe vinaweza kufunguliwa endapo watu wasiokuwa wanafamilia moja wataisitizwa kujiweka umbali wa futi 6 na wengine.
- Maktaba na majumba ya kumbukumbu yanaweza kufungua mnamo Juni 8
- Makusanyiko ya kijamii ya ndani na matukio ya watu 10 au chini inaruhusiwa.
- Makusanyiko ya nje ya kijamii na matukio zinaruhusiwa iwapo watu wataisitizwa kujiweka umbali wa futi 6 na wenzao na mkutano huo uwe wa watu 100 au chini
- Madarasa ya mazoezi ya nje ya mwili, mazoezi ya riadha, vikao vya mafunzo au michezo vinaweza kuendelea ikiwa washiriki, makocha na watazamaji wasio wanafamilia moja wataisitizwa kujiweka umbali wa futi 6 na wengine, na hivyo vifaa na vyombo vinachangiwa kwa kiwango cha chini iwezekanavyo.

BIASHARA AMBAZO HAZITAFUNGULIWA

- Jumba la mazoezi ya ndani, vituo vya mazoezi ya mwili, vituo vya starehe, vituo vya michezo na vituo/studio za mazoezi
- Huduma zisizo za muhimu sana za utunzaji wa kibinafsi pamoja na nywele, chemichemi za madini ya kijadi zinodhaniwa kuwa zinatoa afya njema kucha, ubadilishaji wa ngozi, ujumbe wa tatuu, Sanaa za mwili, na huduma za kutoboa.
- Kasino na sehemu za mashindano ya mbio zilizosajiliwa na Bodi ya Udhhibiti wa Michezo ya Michigan
- Huduma/vituo vya ndani, au huduma/vituo vya nje vinavyohusiana kwa ukaribu wa kugusana na watu, kama vile mbuga za burudani, arcades, arcades, kumbi za bingo, bowling alleys, vituo vya ndani vya kukweea, studio za densi, sehemu za michezo ya utelezi, na mbuga za trampoline.

Habari za hivi karibuni za COVID-19 zinapatikana kwanye [Michigan.gov/Coronavirus](https://www.michigan.gov/Coronavirus) and [CDC.gov/Coronavirus](https://www.cdc.gov/Coronavirus). Kwa wale walio na maswali kuhusu hatua za serikali kupunguza kuenea kwa ugonjwa wa corona, tafadhali ita COVID-19 kwa 1-888-535-6136 kati ya 8 asubuhi na 5 jioni kila siku.